

Maombi ni moja ya mambo yaliyochukuliwa kuwa ni magumu kiasi cha kufikia watu kutenga watu na kuwaita waombaji au watu wa kuwaombea. Katika siku za leo inaonekana kama vile maombi ni kwa ajili ya watu fulani wachache waliotengwa kwa ajili hiyo, wengi huzani maombi ni kwaajili ya wachungaji , watu wenye huduma n.k na wao hujitoa katika nafasi za kuwa waombaji.

Leo nina ujumbe kwa ajili yako kwamba maombi ni kwaajili ya wanadamu wote walio hai, kila mtu anapaswa kuomba huna mtu wa kuwajibikia maisha yako zaidi ya wewe binafsi, unapaswa kuomba tena pasipo kukoma.

Zamani kabla ya Yesu Kristo kuja ulimwenguni ilikuwa ni makuhani tu walioruhusiwa kusogea mbele za Mungu na kufanya maombi lakini Kristo alipokuja aliondoa kiambaza na amefanyika daraja, kila mtu anayemwamini anaweza kwenda mbele za Baba na kuomba lolote, Waefeso 2:14, 18 Kwa maana yeye ndiye amani yetu, alyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga, ¹⁸ kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja.

Ni wajibu wako kwenda mbele za Baba na kuomba, kuomba sio hiari ni lazima kwa yeyote anayemkiri Yesu kuwa ni Bwana. Maombi ni ya muhimu mno kwa mwamini. Kwasababu maombi ni namna ya kumsihi Mungu ashughurike na vyote unavyovihitaji badala yako.

Lakini huwenda wengi wetu tumefanya sana maombi na ikafika kipindi tukakata tamaa kwasababu hatukuona matokeo ya kile tulichokuwa tunamuomba Mungu. Biblia iko wazi juu ya hili kwamba wakati

mwingine tunaweza kuomba na tusipate majibu ya maombi yetu na imetoa na sababu.

Yakobo 4:3 Hata mwaomba lakini hampati kwasababu mwaomba vibaya , ili mvitumie kwa tamaa zenu.

Kutopata majibu ni sababu kubwa inayowafanya wengi wakate tamaa na kuacha kuomba, lakini kukata tamaa sio suruhisho la matatizo walio nayo, njia pekee ni kutafuta majibu ya kwanini maombi yako hayajibiwi.

Katika kitabu hiki kuna majibu ya maswali yako yaliyokusumbua muda mrefu kwanini maombi yako hayajibiwi, kwanini haupaswi kukata tamaa kwa habari ya maombi na namna bora ya kuomba mbele za Baba ili maombi yako yapate kibari.

Mungu wetu ni Mungu wa utaratibu na kanuni, hivyo ameweka kanuni za namna ya kukufanya wewe kama mtoto wake ufanikiwe, katika kitabu hiki tutajifunza kanuni za kukufanikisha kupitia maombi. Ipo misingi muhimu ambayo kabla hujaomba unatakiwa uijenge kwanza ili kupata uhakika wa matokeo ya maombi yako.

Nimejifunza hili kwa baba yangu wa kiroho na kwangu nimelishuhudia kuwa kuna wakati unaweza kuomba maneno machache tu kwa kuzingatia misingi kadhaa ya maombi na maombi yako yakapata kibari mbele za Mungu na ukaona matokeo juu ya kile ulichoomba, hivyo si jambo la wewe unahitaji nini ila ni namna ulivyozitumia kanuni.